## NI DALILI ZIPI ZA ULEMAVU WA KUSIKIA KWA WATU WAZIMA NA WATOTO?

- Mtu anaweza kuwa na Usikivu hafifu au Uziwi. Hali hii inaweza kujitokeza kwenye Sikio moja au Masikio yote mawili
- Ulemavu wa Kusikia hauna Athari yoyote kwenye mfumo wa Akili ya mtu
- Watu wazima: Mtu anaweza kushindwa kusikia sauti yoyote vizuri au kumsikia mtu anayemuongelesha. Hali hii inaweza kutafsiriwa vibaya na mzungumzaji.
- **Watoto:**
  - *Kushindwa kujibu au kuonesha hali dhaifu ya Muitikio wa Sauti yoyote inayosikika kwenye Mazingira*
  - *Kutomgeukia Mlezi pale anapoongeleshwa*
  - *Kutoiga sauti au Matamshi (kuanzia Umri wa wa miezi 3-6)*
  - *Kubwabwaja kusiko kwa kawaida au kushindwa kutamka maneno ya awali (kuanzia Umri wa miezi 6-10)*



## UNAWEZAJE KUSAIDIA MAKUZI YA LUGHA NA MATAMSHI KWA MTOTO MWENYE ULEMAVU WA KUSIKIA?

- Kama ilivyo kwa Watoto wengine, Watoto wenye Ulemavu wa Kusikia wana uhitaji wa Kuwasiliana na wengine
- Watoto wanajifunza Lugha kwa njia ya kucheza na kuzungumza na Walezi wao. **Usiache kuzungumza na Mtoto wako hata kama hakusikii vizuri!**
- Mlezi anaweza kutumia njia mbalimbali za kimawasiliano ili kumsaidia Mtoto mwenye Ulemavu wa Kusikia kumuelewa na kufuatilia kwa usahihi kile anachomuongelesha.
- **Njia hizi za kimawasiliano zinaweza kutumiwa tunapowasiliana na Watu wenye Ulemavu wa Kusikia kwa ujumla:**
  - ***Kumgusa*** *Mtoto/Mtu mzima unapotaka kuwasiliana naye ili kumuwezesha kuwa makini na kile unachotaka kuwasiliana naye*
  - ***Kuwa karibu*** *na Mtoto/Mtu mzima unapowasiliana naye*
  - ***Kumtazama usoni*** *Mtoto/Mtu mzima unapowasiliana naye*
  - ***Kupunguza au kuondoa Sauti yoyote*** *(kwenye Mazingira) ambayo inaweza kuondoa Utulivu kati yenu*
  - *Kuzungumza pole pole*
  - ***Kuzungumza kwa namna tofauti tofauti*** *ambazo zitamfanya Mtoto/Mtu mzima kukuelewa (sauti, melodi)*
  - ***Kukata kata Mazungumzo*** *ili kumuwezesha Mtoto/Mtu mzima kutafakari kile ulichozungumza*
  - ***Kutumia Alama mbalimbali usoni na vitendo*** *ili kuwezesha kile unachozungumza kueleweka*

## NI KWA JINSI GANI UWEZO WA KUSIKIA UNASAIDIA MAKUZI YA LUGHA NA MATAMSHI KWA MTOTO?

- Uwezo wa Kusikia una mchango mkubwa katika Makuzi ya Lugha na Matamshi kwa Mtoto
- Usikivu unamuwezesha Mtoto kushirikiana na Mlezi kwa njia mbalimbali na mazingira kwa ujumla, Mambo ambayo ni muhimu sana katika Makuzi ya Lugha na Matamshi
- Kwa njia ya Kusikia, Mtoto anaweza kutambua na kujifunza kutumia:
  - ***Sauti mbalimbali***
  - ***Melodi ya Sauti***
  - ***Sauti za Matamshi yao wenyewe na kubwabwaja***
  - ***Kanuni na Miundo mbalimbali ya Lugha mama***
  - ***Sauti na Matamshi kuzungumzia mahitaji yao***



## NI KWA JINSI GANI ULEMAVU WA KUSIKIA UNAWEZA KUATHIRI MAKUZI YA LUGHA NA MATAMSHI KWA MTOTO?

- Ulemavu wa Kusikia unaweza kuchelewesha makuzi ya Lugha na Matamshi kwa Mtoto. Hii inategemea ukubwa wa tatizo na aina ya Ulemavu wa Kusikia
- Ulemavu wa Kusikia unaweza kumfanya Mtoto kushindwa:
  - *Kujifunza jinsi ya kuwasiliana au kuwasilisha Mahitaji yake kwa wengine*
  - *Kujifunza na kutamka Sauti za Maneno, Melodi na Maneno ya lugha yake*
  - *Kujifunza jinsi ya kutofautisha/kutumia Sauti katika Mawasiliano*
  - *Kushirikiana na watu wengine katika Mazingira yake (mf. Mlezi au Mgeni)*




## NI MAMBO GANI YANAWEZA KUSABABISHA ULEMAVU WA KUSIKIA?

- Kuumia sikioni (mf. Vitu vyenye ncha kali, kumpiga mtu kofi (kwa nguvu) sikioni)
- Maambukizi Masikioni/Koromeo (kwa muda mrefu)
- Maambukizi ya Magonjwa na Virusi (wakati wa ujauzito)
- Madhara ya Dawa (kwa Mtoto au Mama wakati wa Ujauzito)
- Athari za kurithi (genetic)
- Kelele zilizo kithiri
- Uchafu, Wadudu au Vitu ndani ya Sikio
- Uchafu/Asali sikio iliyokithiri

## NIFANYE NINI ILI KUEPUKA ULEMAVU WA KUSIKIA?

- **Epuka kuumia sikioni**
- **Uwe mwangalifu unaposafisha Sikio: Usitumie vitu vyenye ncha kali**
- **Epuka kelele zilizokithiri**
- **Utafute Ushauri wa kitaalamu (hospitalini) endapo Mtoto wako ana Maumivu ya Sikio, Puani au kwenye Koromeo**




## NI WAKATI GANI WA KUTAFUTA USHAURI HOSPITALINI AU WA KIDAKTARI?

- Pale unapogundua kuwa Mtoto wako hasikii vizuri
- Sababu nyingine ni:
  - ***Maumivu ya Sikio yaliyokithiri***
  - ***Majimaji (Damu, Usaha) unaotoka sikioni***
  - ***Harufu mbaya sikioni***
  - ***Maambukizi sikioni, kuuumia sikioni, vitu visivyotakiwa sikioni)***
  - ***Kupoteza Usikivu gafla***
  - ***Maumivu ya Sikio, Puani au kwenye Koromeo***



## MAELEZO KWA AJILI YA MAWASILIANO

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

**KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE**
**SIMU:**

**0754 844 777**
**0714 157 837**

**MHUSIKA:**

______________________________

______________________________

Sebastian Kolowa Memorial University SEKOMU — IRENTE CHILDREN'S HOME — Leibniz Universität Hannover

© 2019 Prof. Dr. Ulrike Lüdtke,
Leibniz Universität Hannover
– All Rights Reserved –

ulrike.luedtke@ifs.uni-hannover.de

Niedersächsisches Ministerium für Soziales, Gesundheit und Gleichstellung

Kipeperushi hiki kimetengenezwa kwa msaada wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Afya na Fursa Sawa ya Jimbo la Lower Saxony, Ujerumani

## MAFUNZO YA MALEZI YA AWALI NA MAKUZI YA MATAMSHI NA LUGHA KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE, FEB 2018 – SEP 2019




# ULEMAVU WA KUSIKIA

Tunawashukuru washiriki wote wa Mafunzo kwa kutunga maudhui na kupigapicha mbalimbali zilizomo kwenye kipeperushi hiki.

Kwa sababu za kimaadili, tunadiriki kutoonyesha sura za watoto walioko kwenye picha.